The University of Osaka
Institutional Knowledge Archive

| | |
|---|---|
| Title | Miundo ya Dhamira Matilaba na Dhamira Amri katika Kichaani |
| Author(s) | Takemura, Keiko |
| Citation | スワヒリ＆アフリカ研究. 2015, 26, p. 170-180 |
| Version Type | VoR |
| URL | https://doi.org/10.18910/72976 |
| rights | |
| Note | |

*The University of Osaka Institutional Knowledge Archive : OUKA*

https://ir.library.osaka-u.ac.jp/

The University of Osaka

# Miundo ya Dhamira Matilaba na Dhamira Amri katika Kichaani[1]

TAKEMURA Keiko

## 0. Utangulizi

Kama tunavyojua Kiswahili ni lugha inayosemwa katika nchi nyingi za Afrika ya Mashariki na tena ambayo imefanyiwa tafiti nyingi mbalimbali kuliko lugha nyingine nyingi za bara la Afrika, lakini bila shaka lugha hii si lugha ya aina moja peke yake tu bali lugha yenyewe ina lahaja nyingi sana. Tangu zamani watafiti wengi wamegawanya na kutaja idadi ya lahaja za Kiswahili kuwa ni 20 mpaka 24 hivi (Stigand 1915, Bryan 1959, Mkude 1983, Nurse & Hinnebusch 1993). Katika makala hii tutazungumzia lahaja moja ya kisiwa cha Unguja. Lahaja hii tuiite Kichaani kwa sababu inasemwa katika kijiji cha Chaani kilichoko katika Wilaya ya Kaskazini 'A', Mkoa wa Kaskazini, kisiwani Unguja.

Kijiji cha Chaani kiko Kaskazini-mashariki ya Mji Mkongwe, masafa yake ni kilomita 40 hivi kutoka mjini. Kijiji hicho inasemekana kuwa kilijengwa na watu wanaotoka kisiwa cha Tumbatu. Wanakijiji wengi wametanabahi kama Kiswahili wanachosema na Kiunguja-Mjini kinatofautiana. Kwa kweli, kutokana na matokeo ya utafiti wangu[2], imehakikishwa kuwa Kichaani na Kiunguja-Mjini kinatofautiana hata kisarufi na kimsamiati.

Katika makala hii tutaangalia miundo ya dhamira matilaba na dhamira amri ya Kichaani. Katika mifano ya sentensi yenye muundo wa dhamira matilaba bila shaka inajitokeza dhamira dhahiri, kwa hivyo tutazungumzia muundo wake pia. Na tunapoandika Kichaani, tunafuata kanuni ya kuandika Kiswahili Sanifu. Ili kuhakikisha tofauti baina ya Kichaani na Kiswahili Sanifu, tutaonyesha mifano ya sentensi za Kichaani pamoja na tafsiri zake kwa Kiswahili Sanifu. Mifano yenye herufi 'a' ni sentensi za Kichaani, na yenye herufi 'b' ni za Kiswahili Sanifu. Na tafsiri zake za sentensi kwa Kiingereza zinaambatishwa juu.

## 1. Muundo wa Dhamira Dhahiri

Katika Kichaani, muundo wa dhamira dhahiri ni hivi:

| kiambishi-kiima – kiambishi-njeo – kiambishi-yambwa – mzizi wa kitenzi – kiambishi-nyambulishi – kiishio |
|---|

[1] Makala hii, msingi wake umeandikwa kwa Kijapani na makala hiyo ya Kijapani ilichapishwa katika Na. 25 ya jarida hili *Swahili & African Studies*. Ukitaka kujua habari zaidi, angalia kwenye marejeo ya makala hii.

[2] Nilifanya utafiti wangu huko kijijini Chaani mwezi wa 8 mwaka 2011, mwezi wa 8 mwaka 2012 na mwezi wa 8 mwaka 2013. Nitaandika makala nyingine juu ya matokeo ya utafiti huu.

(1) 'You cook for me.'

a. Ku-na-ni-pik-i-ya.

SM2SG-PRS-OM1SG-cook-APPL-BF

b. U-na-ni-pik-i-a.

SM2SG-PRS-OM1SG-cook-APPL-BF

Katika muundo huu, kiambishi-kiima, kiambishi-njeo, mzizi wa kitenzi na kiishio ndizo mofimu zisizokosekana. Kiambishi-kiima kinatokea kupatana na kiima cha sentensi na kiambishi-yambwa kinatokea kupatana na yambwa ya sentensi, lakini baadhi ya sentensi hazina kiima chenyewe wala yambwa yenyewe, basi katika sentensi kama hizo kiambishi-kiima na kiambishi-yambwa kinafanya kazi ya kiwakilishi. Hasa ikiwa kiambishi-kiima ama kiambishi-yambwa ni kiambishi-nafsi, katika sentensi kiwakilishi-nafsi hakitokei kwa kawaida, na kikitokea kinafanya kazi ya kusisitiza.

Ikiwa nomino ya kiima ama ya yambwa ina maana ya 'kiumbe', hata kama nomino hii si ya ngeli ya 1 (umoja) au 2 (wingi), kiambishi-kiima ama kiambishi-yambwa sharti kiwe cha ngeli ya 1 au 2. Ikiwa sentensi yenyewe ni ya kukanusha, kiambishi-kiima lazima kiwe cha kukanusha.

Kinachoonyesha njeo ni kiambishi-njeo, lakini kwa baadhi ya njeo hata kiishio kinabadilika. Kwa mfano sentensi ya njeo ya wakati uliopita ina kiishio ambacho ni vokali sawa na vokali ya mwisho kabisa ya mzizi wa kitenzi. Tutaonyesha njeo zote za Kichaani katika jedwali lifuatalo. Kwa kawaida kiishio ni vokali moja, lakini ili kuepusha mfululizo wa vokali kadhaa, ikiwa sauti ya mwisho ya mzizi wa kitenzi ni vokali ama sauti ya mwisho ya kiambishi-nyambulishi ni vokali, /y/ inaingizwa kabla ya kiishio. Katika jedwali lifuatalo '-V' maana yake ni vokali sawa na vokali ya mwisho kabisa ya mzizi wa kitenzi.

＜Jedwali la 1: viambishi-njeo na viishio vya Kichaani＞

| kiambishi-njeo | |
|---|---|
| -na- | wakati uliopo |
| -ta- | wakati ujao |
| -ø- | wakati uliopita |
| -e- | ukanushi wa wakati uliopita |
| -ma- | hali timilifu |
| -sha- | hali timilifu kabisa |
| -ja- | ukanushi wa hali timilifu |
| -ka- | hali ya kufuata, sharti, wakati mmoja |
| -hu- | hali ya mazoea |
| -nge- | hali ya sharti lisilotimia |
| -ngali- | hali ya kuendelea |

| kiishio | |
|---|---|
| -a | msingi |
| -V | ukanushi wa wakati uliopo<br>wakati uliopita |
| -e | dhamira matilaba |

(2) 'I studied Swahili.'

a. Ni-som-o Kiswahili

SM1SG-study-PstF Swahili7

b. Ni-li-som-a Kiswahili

SM1SG-PST-study-BF Swahili7

Katika sentensi ya wakati uliopita kiishio chake ni vokali sawa na vokali ya mwisho kabisa ya mzizi wa kitenzi[3], lakini kama tulivyotaja hapo juu, ili kuepusha mfululizo wa vokali kadhaa, ikiwa sauti ya mwisho wa mzizi wa kitenzi ni vokali, /y/ inaingizwa kabla ya kiishio kama katika mfano (3).

(3) 'She/he bought a book.'

a. Ka-nunu-yu buku.

SM3SG-buy-PstF book5

b. A-li-nunu-a kitabu.

SM3SG-PST-buy-BF book7

Lakini ikiwa sauti ya mwisho kabisa ya mzizi wa kitenzi ni vokali 'e' au 'i', /l/ inaingizwa kabla ya kiishio kama katika mfano (4) na (5).

(4) 'We brought up Juma.'

a. Tu-m-le-le Juma.

SM1PL-OM3SG-bring up-PstF Juma

b. Tu-li-m-le-a Juma.

SM1PL-PST-OM3SG-bring up-BF Juma

(5) 'You cried.'

a. Mu-li-li.

SM2PL-cry-PstF

b. A-li-li-a.

SM2PL-PST-cry-BF

## 2. Muundo wa Dhamira Matilaba

Tukitaka kuomba, kutoa mashauri, kushawishi, n.k., tunatumia dhamira matilaba. Muundo wa dhamira matilaba ni hivi:

Uyakinishi:

kiambishi-kiima – kiambishi-yambwa – mzizi wa kitenzi – kiishio cha dhamira matilaba

[3] Whiteley (1959) ametaja kuwa hata katika Kimtang'ata muundo wa sentensi ya wakati uliopita ni vilevile. Kimtang'ata kinasemwa si visiwani bali barani, kwa hivyo inasemekana kwamba unahitajika utafiti wa dhati wa lahaja nyingine nyingi za sehemu za bara hasa mkabala wa kisiwa cha Unguja.

Ukanushi:

| kiambishi-kiima – kiambishi-kanushi – kiambishi-yambwa – mzizi wa kitenzi – kiishio cha dhamira matilaba |
|---|

(6) 'Let me give you a pen.'

a. Ni-ku-p-e kalamu.
SM1SG-OM2SG-give-SBJF pen9

b. Ni-ku-p-e kalamu.
SM1SG-OM2SG-give-SBJF pen9

(7) 'Drink this water.'

a. U-nyw-e maji yano.
SM2SG-drink-SBJF water6 DEMN6

b. U-nyw-e maji haya.
SM2SG-drink-SBJF water6 DEMN6

(8) 'Let's go home.'

a. Tu-rudi nyumbani.
SM1PL-go back home17

b. Tu-rudi nyumbani.
SM1PL-go back home17

(9) 'We won't go home.'

a. Tu-si-rudi nyumbani.
SM1PL-Neg-go back home17

b. Tu-si-rudi nyumbani.
SM1PL-Neg-go back home17

Katika muundo ulioonyeshwa juu kiambishi-yambwa si lazima kiwepo mara zote. Kutokana na mfano (8) na (9) inadhihirika wazi kwamba kitenzi kilichoazimwa kutoka lugha nyingine hakihitaji kuambatishwa kiishio cha dhamira matilaba.

(10) 'Please make breads for me.'

a. U-ni-tend-e-le mikate.
SM2SG-OM1SG-make-APPL-SBJF bread4

b. U-ni-tengenez-e-e mikate.
SM2SG-OM1SG-make-APPL-SBJF bread4

(11) 'Don't let me help you.'

a. Ni-si-ku-saidi-le.
SM1SG-Neg-OM2SG-help-SBJF

b. Ni-si-ku-saidi-e.
SM1SG-Neg-OM2SG-help-SBJF

(12) 'Let's sit down here.'

a. Tu-ka-le pano.

SM1PL-sit down-SBJF DEMN16

b. Tu-ka-e hapa

SM1PL-sit down-SBJF DEMN16

Tukiangalia mifano ya (10), (11) na (12) inafahamika kwamba ikiwa sauti ya mwisho kabisa ya mzizi wa kitenzi ama sauti mwisho kabisa ya kiambishi-nyambulishi ni vokali, /l/ inaingizwa kabla ya kiishio cha dhamira matilaba.

### 3. Muundo wa Dhamira Amri

Wakati tunapotaka kutoa amri, kauli ya dhamira amri inatumika. Tukitaka kumwamuru mtu mmoja, kama ilivyo katika Kiswahili Sanifu, hata Kichaani vilevile muundo wake ni hivi:

mzizi wa kitenzi – kiishio cha msingi

Lakini tukitaka kuwaamuru watu zaidi ya wawili, muundo wake ni hivi:

mzizi wa kitenzi – kiishio cha msingi – kiambishi-tamati cha wingi

(13) 'Do.'

a. Tend-a.

do-BF

b. Fany-a.

do-BF

(14) '(all of you) Do.'

a. Tend-a-ni.

do-BF-ImpPL

b. Fany-e-ni.

do-BF-ImpPL

(15) 'Leave.'

a. Uk-a.

leave-BF

b. Ondok-a.

leave-BF

(16) '(all of you) Leave.'

a. Uk-a-ni.

leave-BF-ImpPL

b. Ondok-e-ni.

leave-BF-ImpPL

Kama inavyoonyeshwa katika mifano ya (14) na (16), hata tukiongeza kiambishi-tamati cha

wingi katika Kichaani kiishio cha dhamira amri ni cha msingi vilevile ingawa katika Kiswahili Sanifu kiishio kitabadilika kuwa sauti 'e' badala ya 'a'. Na kama tutakavyoona katika mifano (17), (18) na (19) vitenzi vitatu hivi yaani -enda (go), -ja (come) na -leta (bring), vinaonyesha muundo wake wa kipekee katika dhamira amri.

(17) 'Go.' '(all of you) Go.'
a. -enda: Nenda. Nendani.
b. -enda: Nenda. Nendeni.

(18) 'Come.' '(all of you) Come.'
a. -ja: Njo. Njoni.
b. -ja: Njoo. Njooni.

(19) 'Bring.' '(all of you) Bring.'
a. -leta: Lete. Leteni.
b. -leta: Lete. Leteni.

Halafu, tukitaka kutoa amri ya kukataza kufanya jambo fulani, muundo wa dhamira amri utakuwa sawasawa na muundo wa ukanushi wa dhamira matilaba.

(20) 'Don't drink this water.'
a. U-si-nyw-e maji yano.
SM2SG-Neg-drink-SBJF water6 DEMN6
b. U-si-nyw-e maji haya.
SM2SG-Neg-drink-SBJF water6 DEMN6

(21) 'Don't listen to her/him.'
a. M-si-m-sikiz-e.
SM2PL-Neg-OM3SG-listen-SBJF
b. M-si-m-sikiliz-e.
SM2PL-Neg-OM3SG-listen-SBJF

## 4. Kulinganisha Muundo wa Dhamira Matilaba na Dhamira Amri

Kuna tofauti kubwa ya matumizi ya dhamira matilaba na dhamira amri. Dhamira matilaba inaonyesha maana ya 'kuomba' ama 'kuagiza kwa upole' lakini dhamira amri inaonyesha maana ya 'kuamuru'. Tuhakikishe kwa kuangalia mifano ifuatayo.

(22) 'Would you please give me a glass of water?'
a. U-ni-p-e maji gilasi moja.
SM2SG-OM1SG-give-SBJF water6 glass9 adjective 'one'

b. U-ni-p-e maji gilasi moja.

SM2SG-OM1SG-give-SBJF water6 glass9 adjective 'one'

(23) 'Give me a glass of water.'

a. Ni-p-a maji gilasi moja.

OM1SG-give-BF water6 glass9 adjective 'one'

b. Ni-p-e maji gilasi moja.

OM1SG-give-SBJF water6 glass9 adjective 'one'

Mfano wa (22) ni dhamira matilaba na mfano wa (23) ni dhamira amri. Kutokana na (23) inasemekana kwamba ikiwa yambwa ni nafsi ya kwanza na umoja yaani kama kusema 'wewe, unifanyie mimi xxxxx', katika Kichaani kiishio cha dhamira amri kitakuwa cha msingi. Hii inaonyesha tofauti kubwa sana na Kiswahili Sanifu. Na tena kama tutakavyoona katika mfano wa (25), kiambishi-yambwa kikiwa nafsi ya kwanza na wingi, kiishio cha dhamira amri hakitofautiani na cha Kiswahili Sanifu.

(24) 'Would you please make bread for us?'

a. U-tu-tend-e-le mikate.

SM2SG-OM1PL-make-APPL-SBJF bread4

b. U-tu-tengenez-e-e mikate.

SM2SG-OM1PL-make-APPL-SBJF bread4

(25) 'Make bread for us.'

a. Tu-tend-e-le mikate.

OM1PL-make-APPL-SBJF bread4

b. Tu-tengenez-e-e mikate.

OM1PL-make-APPL-SBJF bread4

Halafu, tukitaka kuwaomba ama kuwaamuru watu zaidi ya wawili, miundo ya dhamira matilaba na dhamira amri itakuwa kama inavyoonyeshwa katika mifano ifuatayo.

(26) '(all of you) Please give me a pen.'

a. M-ni-p-e kalamu.

SM2PL-OM1SG-give-SBJF pen9

b. M-ni-p-e kalamu.

SM2PL-OM1SG-give-SBJF pen9

(27) '(all of you) Give me a pen.'

a. Ni-p-a-ni kalamu.

OM1SG-give-BF-ImpPL pen9

b. Ni-p-e-ni kalamu.

OM1SG-give-BF(mabadiliko ya sauti)-ImpPL pen9

Kutokana na mfano wa (27) inadhihirika kwamba hata kiima kikiwa nafsi ya pili na wingi, ikiwa kiambishi-yambwa ni nafsi ya kwanza na umoja, katika Kichaani kinaingizwa kiishio cha msingi kabla ya kiambishi-tamati cha wingi. Tuhakikishe kwa kuangalia mifano ifuatayo kwamba hakuna tofauti ya kiishio baina ya Kichaani na Kiswahili Sanifu katika muundo wa dhamira amri usio na kiambishi-yambwa cha nafsi ya kwanza na umoja.

(28) 'Give her/him a pen.'
 a. M-p-e kalamu.
 OM3SG-give-SBJF pen9
 b. M-p-e kalamu.
 OM3SG-give-SBJF pen9
(29) '(all of you) Give her/him a pen.'
 a. M-p-e-ni kalamu.
 OM3SG-give-BF-ImpPL pen9
 b. M-p-e-ni kalamu.
 OM3SG-give-BF-ImpPL pen9
(30) 'Give them a pen.'
 a. Wa-p-e kalamu.
 OM3PL-give-SBJF pen9
 b. Wa-p-e kalamu.
 OM3PL-give-SBJF pen9
(31) '(all of you) Give them a pen.'
 a. Wa-p-e-ni kalamu.
 OM3PL-give-BF-ImpPL pen9
 b. Wa-p-e-ni kalamu.
 OM3PL-give-BF-ImpPL pen9

Sasa tuangalie mifano kadhaa ya sentensi zenye dhamira dhahiri pamoja na dhamira matilaba / dhamira amri.

(32) 'If you get an information, please tell me.'
 a. U-ka-pat-a habari u-ni-ambi-le.
 SM2SG-CONT-get-BF news9 SM2SG-OM1SG-tell-SBJF
 b. U-ki-pat-a habari u-ni-ambi-e.
 SM2SG-CONT-get-BF news9 SM2SG-OM1SG-tell-SBJF
(33) 'If you get an information, tell me.'
 a. U-ka-pat-a habari ni-ambi-ya.
 SM2SG-CONT-get-BF news9 OM1SG-tell-BF
 b. U-ki-pat-a habari ni-ambi-e.
 SM2SG-CONT-get-BF news9 OM1SG-tell-SBJF

(34) 'If you come again, please bring me a spoon.'

a. U-ka-j-a tena u-ni-let-e-le kijiko.

SM2SG-CONT-come-BF again SM2SG-OM1SG-bring-APPL-SBJF spoon7

b. U-ki-j-a tena u-ni-let-e-e kijiko.

SM2SG-CONT-come-BF again SM2SG-OM1SG-bring-APPL-SBJF spoon7

(35) 'If you come again, bring me a spoon.'

a. U-ka-j-a tena ni-let-e-ya kijiko.

SM2SG-CONT-come-BF again OM1SG-bring-APPL-BF spoon7

b. U-ki-j-a tena ni-let-e-e kijiko.

SM2SG-CONT-come-BF again OM1SG-bring-APPL-SBJF spoom7

(36) 'She/he told us "let's run".'

a. Ka-tu-ambi-li "tu-pig-e mbiro."

SM3SG-OM1PL-tell-PstF SM1PL-hit-SBJF speed

b. A-li-tu-ambi-a "tu-pig-e mbio."

SM3SG-PST-OM1PL-tell-BF SM1PL-hit-SBJF speed

(37) 'She/he forbade us "(all of you) don't run".'

a. Ka-tu-kataz-a "m-si-pig-e mbiro.

SM3SG-OM1PL-forbid-PstF SM2PL-Neg-hit-SBJF speed

b. A-li-tu-kataz-a "m-si-pig-e mbio."

SM2SG-PST-OM1PL-forbid-BF SM2PL-Neg-hit-SBJF speed

Kutokana na mifano ya (33) na (35), inadhihirika kwamba katika Kichaani ikiwa kiambishi-yambwa ni nafsi ya kwanza na umoja, kiishio cha dhamira amri ni cha msingi.

## 5. Hitimisho

Katika makala hii tumeangalia miundo ya dhamira matilaba na dhamira amri ya Kichaani kwa kulinganisha na ya Kiswahili Sanifu. Kama tulivyotaja juu, tofauti kubwa sana iliyoko baina ya Kichaani na Kiswahili Sanifu ni kwamba ikiwa kiambishi-yambwa ni nafsi ya kwanza na umoja katika Kichaani kiishio cha dhamira amri si cha dhamira matilaba bali ni cha msingi.

Inasemekana kuwa ili kuhakikisha kama kuna tofauti kama hii baina ya lahaja zinazozungumzwa katika vijiji vingine vilivyoko karibu na kijiji cha Chaani na Kiswahili Sanifu, tunahitaji kufanya utafiti zaidi na zaidi katika eneo kubwa la Mkoa wa Kaskazini, Kisiwani Unguja, na kulinganisha na kuchambua matokeo yake.

* Utafiti wangu huu uliendeshwa kwa msaada wa kifedha wa Wizara ya Elimu ya Japani wa mwaka wa kielimu 2011-2013. Mradi wetu wa utafiti (Namba ya mradi:(B) 23320086, Kiongozi wa mradi:TAKEMURA Keiko, Profesa Mshiriki, Chuo Kikuu cha Osaka) unaitwa 'Utafiti wa Lahaja za Kiswahili, Afrika ya Mashariki'.

### Shukrani

Kila mara nilisaidiwa na mhojiwa Bi. ‘M’ mwenye umri wa miaka 84 hivi (mwaka 2013) aliyekaa katika mtaa mmoja wa Chaani. Nisingekutana naye bila shaka nisingeweza kuandika makala hii, namshukuru kwa dhati yangu hasa. Na tena kila mara nilisaidiwa sana na msaidizi wangu Mwl. ‘H’ pamoja na familia yake. Nilikaa na familia yake kwa muda wote nilipokuwa Chaani. Kwa msaada wao mkubwa niliweza kufanya utafiti wangu bila ya tatizo lolote, ninawashukuru mno. Halafu lazima nitaje jina lake Mwl. Zainabu kwa msaada wake mkubwa. Amenipitia na kunirekebishia makala hii kwa dhati. Ninamshukuru sana sana.

Mwishoni niongeze kutaja kwamba ikiwa kuna makosa ama kasoro ya maandiko ya makala hii, bila shaka ni wajibu wangu, si wajibu wao mhojiwa na wasaidizi wangu.


### Vifupisho

| | |
|---|---|
| - | mpaka wa mofimu |
| 1SG, 1PL | nafsi ya kwanza-umoja, nafsi ya kwanza-wingi |
| 2SG, 2PL | nafsi ya pili-umoja, nafsi ya pili-wingi |
| 3SG, 3PL | nafsi ya tatu-umoja, nafsi ya tatu-wingi |
| APPL | kiambishi-nyambulishi-utendea |
| BF | kiishio cha msingi |
| CONT | njeo ya hali ya kuendelea |
| DEMN | kiwakilishi kionyeshi-karibu na msemaji |
| ImpPL | kiambishi-tamati cha wingi cha dhamira amri |
| Neg | kiambishi-kikanushi |
| OM | kiambishi-yambwa |
| PRS | njeo-wakati uliopo |
| PST | njeo-wakati uliopita |
| PstF | kiishio cha wakati uliopita |
| SBJF | kiishio cha dhamira matilaba |
| SM | kiambishi-kiima |

### Marejeo


Bryan, M. A. 1959. “Swahili Group”. *The Bantu Languages of Africa*. pp.126-129. Oxford University Press.

Mkude, Daniel J. 1983. “Mtawanyiko wa Lahaja za Kiswahili”. *Makala za Semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili I - Lugha ya Kiswahili*. pp.62-83. Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Nurse, D. & T. J. Hinnebusch. 1993. *Swahili and Sabaki: A Linguistic History.* University of California Press.

Stigand, C. H. 1915. *A Grammar of Dialectic Changes in the Swahili Language*. Cambridge University Press.

Stude, Traute. 1995. “Language Change and Language Maintenance in the Island of Tumbatu”. *Lugha, Utamaduni na Fasihi Simulizi ya Kiswahili.* pp.83-117. TUKI, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

TAKEMURA, Keiko. 2014. “On Subjunctive and Imperative Forms of Kichaani”. *Swahili & African Studies* 25. 120-129. (in Japanese)

Whiteley, W. H. 1956. *Ki-mtang’ata: A Dialect of the Mrima Coast - Tanganyika.* East African Swahili Committee, Makerere College, Kampala.